



UHURU

ISSN 0876-3896 Na. 21733 Alhamisi Februari 6, 2014 Bei TSH. 700

MCHAKATO WA KATIBA

Mataifa ya nje

yajipenyeza

HABARI
UK. 4

Mataifa ya nje yajipenyeza

NA MWANDISHI WETU

MPANGO mkakati wa CHADEMA kuingilia mchakato wa katiba kwa kutumia baadhi ya taasisi zisizokuwa za kiserikali umefichuka, baada ya kuanzisha yake inayoshirikiana na za nje kufanya mdahalo wa katiba mpya.

Taasisi hiyo Tanzania Development Initiative Programme (TADIP), leo inafanya mdahalo 'Maendeleo Dialogue' kwa kushirikiana na taasisi kutoka Ujerumani ya Konrad-Adenauer-Stiftung Tanzania (KAS).

KAS imekuwa ikiisaidia CHADEMA kuandaa midahalo na kuendesha semina za ndani ya chama hicho; na kuandaliwa mdahalo huo kupitia TADIP

kunaelezwa ni moja ya mikakati ya chama hicho katika katiba mpya ya kupata sauti ya NGO zingine.

"Mialiko ilishasambazwa kwa watu ili waje kutoa maoni kwa TADIP kwa kuwa ndiyo walioanzisha mdahalo huu. Ukweli ni kwamba hii ni NGO ya CHADEMA na ipo kwa malengo maalumu, hata mkurugenzi anafanya kazi ya sheria BAVICHA," kilisema chanzo chetu cha habari.

Taarifa hiyo ilisema licha ya kuwa mwanasheria wa BAVICHA, John Mallya, amekuwa akitumika katika dawati la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, akiwa mmoja wa viongozi na wapanga mikakati na amepewa nafasi hiyo ili kuhakikisha anakisaidia chama

hicho.

TADIP ilianzishwa 2011 na uongozi wa juu wa chama hicho, ukiongozwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu, Dk. Willibrod Slaa, ambapo Oktoba 14, mwaka huo, kuliundwa bodi ya wakurugenzi, iliyopewa majukumu kadhaa, ikiwemo kuandaa midahalo na makongamano kupitia TADIP.

Bodi ya wakurugenzi inaundwa na watu sita, akiwemo mmoja wa viongozi wa NGO ya Kiwohede, ambaye amepewa kazi ya kuhakikisha taasisi hiyo inaungwa mkono na NGO zingine, na amehidiwa kupewa wadhifa ndani ya chama hicho.

Licha ya Mallya, wajumbe wengine wa bodi hiyo ni

mfanyakazi wa benki moja nchini, wafanyabiashara, mwanahabari na ofisa wa ubalozi wa Canada, ambaye amepewa jukumu la kutafuta vyanzo vingine vya mapato (majina yao yanahifadhiwa).

Kwa mujibu wa mwaliko wa mdahalo huo, mada kuu ni Katiba Moja kwa Watanzania Wote na utafanyika jijini Dar es Salaam.

Kuanzishwa kwa taasisi hiyo kuliripotiwa kwa mara ya kwanza na gazeti la Mzalendo, ambalo ni dada na Uhuru Februari 12, 2012, wakati huo ilipewa jukumu la kuiunganisha CHADEMA na NGO na kutoa matamko ya kuipongeza pale panapojitokeza mambo yanayokizungumzia chama hicho.

Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho,

John Mnyika, alipotafutwa kuzungumzia mdahalo huo, hakupatikana, huku Ofisa Habari wa chama hicho, Tumaini Makene, akisema hawezi kuzungumza chochote kwa kuwa alikuwa nje ya ofisi kwa muda mrefu.

Mallya kwa upande wake alisema ni kweli wameandaa mdahalo na taasisi iliyouandaa haina uhusiano na CHADEMA.

"Ni kweli tuna mdahalo na tumegawa mialiko sehemu mbalimbali lakini taasisi yetu haihusiani na CHADEMA," alisema Mallya.

TADIP ilianzishwa baada ya NGO ya awali ya ERIESA kukosa wafadhili na kushindwa kutimiza majukumu yake, ambayo ilikuwa chini ya Victor Kimesera ■